## Je, Connect Care inabadilishaje utunzaji wangu? (How does Connect Care change my care?)

Unaweza kutarajia utunzaji sawa wa hali ya juu, lakini unaweza kuona tofauti chache, kama vile kuona watoa huduma wako wakitumia kompyuta zaidi na vifaa vinavyoshikiliwa kwa mkono. Tunavitumia kufuatilia utunzaji wako.

Connect Care itakupa kipaumbele kwa:

- Kukupa ufikiaji unapohitaji wa maelezo yako ya afya kupitia zana ya mtandaoni ya MyAHS Connect
- Kukuruhusu kuingiliana na timu yako ya utunzaji na kusimamia maelezo katika rekodi yako ya afya
- Kuboresha mawasiliano na watoa huduma wako wa afya
- Kuzipa timu za huduma ya afya picha kamili zaidi ya afya yako
- Kuipa timu nzima ya afya maelezo bora zaidi katika safari yako ya utunzaji

Ili kupata maelezo zaidi, tembelea **ahs.ca/connectcare**

## MyAHS Connect inaweka maelezo yako ya afya mikononi mwako (MyAHS Connect puts your health information into your hands)

Ikiwa unapokea utunzaji kwenye kituo au kwenye programu kwa kutumia Connect Care na una angalau umri wa miaka 14 na kitambulisho halali, una uwezo wa kuomba ufikiaji wa MyAHS Connect.

Ili kusanidiwa akaunti ya MyAHS Connect:

1. Iambie timu yako ya huduma ya afya kuwa ungependa kufikia akaunti yako ya MyAHS Connect.
2. Fungua Akaunti ya Alberta.ca kwa kutembelea myhealth.alberta.ca/myhealthrecords
3. Ingia kwenye akaunti yako ya MyHealth Records kwa kwenda kwenye myhealth.alberta.ca/myhealthrecords na uweke jina la mtumiaji na nenosiri ulilounda.

MyAHS Connect inakuwezesha:

- Kufikia maelezo na kuongeza maoni au kuhariri maelezo katika chati yako ya Connect Care.
- Kuwasiliana kwa usalama na timu yako ya huduma ya afya ya Connect Care na kushiriki maelezo.
- Kuomba miadi, na kuangalia miadi iliyopita na ijayo.
- Kuwa na ziara za video na timu yako ya utunzaji ikiwa zinapatikana kwenye kliniki yako.

MyAHS Connect inaendeshwa na MyChart® iliyopewa leseni na Epic Systems Corporation, © 1999-2023

Tafadhali kumbuka kuwa, maudhui na maelezo yanayoonyeshwa katika MyAHS Connect yanapatikana kwa Kiingereza pekee.

Alberta Health Services

Swahili



# Kufanya maelezo ya afya kuwa ya kufikiwa kwa urahisi zaidi (Making health information healthier)

## Connect Care

Ili kupata maelezo zaidi, tembelea **ahs.ca/connectcare**

Alberta Health Services



## Picha kamili zaidi ya afya yako (A more complete picture of your health)

Connect Care inabadilisha jinsi Alberta Health Services , washirika wake na wengine wanavyotoa huduma ya afya huko Alberta.

Itahifadhi maelezo yako yote ya afya katika sehemu moja na utakuwa nayo popote ulipo kwenye safari yako ya utunzaji. Utatumia muda mchache ukishiriki "historia" yako na watoa huduma tofauti, kwa kuwa watakuwa nayo tayari.

Ikiwa unapokea huduma kwenye kituo cha Connect Care, uliza timu yako ya huduma ya afya ikupe ufikiaji wa zana mpya ya wagonjwa ya mtandaoni inayoitwa MyAHS Connect. MyAHS Connect itakusaidia kuwa mwanachama wa timu yako ya huduma ya afya anayehusika zaidi, kwa kukuwezesha kuona maelezo yako ya afya kuhusiana na huduma zinazotolewa na AHS, na kukupa uwezo wa kuomba ufikiaji wa maelezo ya afya ya watoto wako na wanafamilia wengine kutoka kwenye akaunti yako.

## Inapatikana kote katika Alberta Health Services na washirika wake (Available across Alberta Health Services and partners)

Connect Care inatekelezwa kwa awamu kote Alberta kwa miaka kadhaa. Itapatikana katika:

- Vituo vya Alberta Health Services, ikiwa ni pamoja na hospitali na vituo vya afya
- Carewest
- CapitalCare
- Covenant Health
- Lamont Health Care Centre
- Alberta Precision Laboratories (APL)
- DynaLIFE Medical Labs
- Kliniki nyingine nyingi na vituo vya kibinafsi

## Imejitolea kulinda faragha yako (Committed to your privacy)

AHS imejitolea kulinda faragha yako na kuweka maelezo yako ya afya salama — ni jambo sahihi kufanya, na ni sheria.

Kila mtu anayetumia Connect Care amepewa mafunzo ya kukupa kipaumbele. Hii ni pamoja na kuheshimu faragha yako kwa kuzuia ufikiaji wa maelezo yako ya afya kwa wale watoa huduma wanaohitaji kuyaona ili kukuhudumia pekee. Connect Care ina zana za kufuatilia mtu anayefikia maelezo yako ili kuhakikisha kuwa sera za maelezo ya afya zinafuatwa.

Connect Care itapunguza pia idadi ya mifumo ya kompyuta tunayotumia, ili tuweze kuzingatia juhudi zetu za usalama wa mtandaoni.

Usalama wa data ni muhimu. Maelezo yote ya mgonjwa huhifadhiwa kwenye seva salama zinazomilikiwa na AHS papa hapa Alberta.

